

DALILI ZA KUJA KWAKE

1st Verse

Dalili za kuja kwake,
Sasa nazo zaonekana,
Aliyoyasema Yesu sasa nayo yametimia.

CHRS: Tujiweke tayari,

Kwenda naye Bwana Yesu.

Siku hiyo ikifika,

Ni furaha kubwa mbinguni X2

2nd Verse

Aliyoyasema Yesu,
sasa nayo yametimia,
Kesheni basi kwa maana hamjui ni siku ipi,

CHRS: Mwenye sikio na asikie,

Neno hili la Bwana Yesu,

Kesheni basi mkiomba,

Asomaye na afhamu x2

Tujiweke tayari kwenda naye Bwana Yesu,

Siku hiyo ikifika ni furaha kubwa mbinguni.

MOYONI MWANGU

Moyoni mwangu nakukaribisha Yesu,
Ufanye makao uzaliwe kwangu.

Nyumba zote zilijaa, haukupata nafasi

kila ulipokwenda haukupata nafasi,

na kwa shida ukazaliwa mwokozi wa ulimwengu,

ilikuthibitisha mauti utaishinda.

Moyoni mwangu nakukaribisha Yesu,

Ufanye makao uzaliwe kwangu.

Ulipokwenda kwa wanadamu haupata nafasi,

kwani mioyo yao imejaa maasi,

kila ulipopita haukupata nafasi,

kwa wanadamu wamejawa na chuki.

Moyoni mwangu nakukaribisha Yesu,

Ufanye makao uzaliwe kwangu.

Baba, mama mkaribishe,

azaliwe ndani yako,

abadilishe maisha yako,

aondoe hizo chuki.

Moyoni mwangu nakukaribisha Yesu,

Ufanye makao uzaliwe kwangu.

MUNGU ASHUKURIWE

Mungu ashukuriwe, kwa kutupenda watoto wake,

Ndiye aliyesema, yeye ni Mungu baba wa yatima,

Alipenda kuwachukua, baba na mama zetu waende kwake,

Yeye sasa ni baba yetu, sisi sio yatima tunae baba

Ameinua watumwa wake, anatumunza baba anatumulinda.

Ooh! Ooh!

Enyi watu wa Mungu, mwaitwa nyote kufanya kazi

Kama mlivyojaliwa, tutunzeni sisi watoto,

Sisi hapa tumekusanywa, tunapata faraja kwa upendo wenu,

Wapo wengine wanateseka, hawana pa kulala wala chakula.
Tunawasihi muwakumbuke, watoto wenzetu hawa watesekao.

Ooh! Ooh!

Mungu alishasema mimi na Mungu baba wa yatima,
Atashuka mwenyewe, kuhudumia watoto wake
Kadri ile mliyofanyia kwa hawa walio wadogo mlifanya kwangu,
Tunzeni basi watoto hawa, na baba yetu naye atawabariki.

YESU SIJUI JINA LINGINE

Yesu sijui lingine
Yesu U mshindi wa milele
Yesu umejaa utukufu
Nitasifu jina lako.

*Sijui jina jingine kwa sababu watupenda,
Sijui jina jingine vilema wanatembea,
Sijui jina jingine na vipofu wanaona
Sijui jina jingine viziwi wanasikia.*

Aha!Yesu

Sijui jingine, Yesu

U mshindi wa milele, Yesu

Umejaa utukufu, Yesu

Nitasifu Jina Lako, Yesu x2 aha!

Yesu sijui lingine
Yesu U mshindi wa milele
Yesu umejaa utukufu

Nitasifu jina lako.

*Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu,
Hata akamtoa mwana wake wa pekee ili
Kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.*

Aah! Yesu

Sijui jingine, Yesu

U mshindi wa milele, Yesu

Umejaa utukufu, Yesu

Nitasifu Jina Lako, Yesu x2 aha

Sijui jina jingine kwa sababu watupenda,

Sijui jina jingine vilema wanatembea,

Sijui jina jingine na vipofu wanaona

Sijui jina jingine viziwi wanasikia.

TWAKUSHUKURU-

1st Verse

Twakushukuru Mungu baba yetu

Kutupatia neema wana wako,

Umetupa jina jema sana,

Kwamba tuitwe watoto wa Mungu,

2nd Verse

Mitaani siyo jina letu,

Mitaani wala si mzazi,

**Mtaani si mlezi wetu,
Jina letu watoto wa Mungu,**

3rd Verse

**Tumepewa majina mengi sana,
Wametuita ati chokoraa,
wametuita watoto wa mitaa,
Jina letu watoto wa Mungu.**

4th Verse

**Asante Mungu kwa kutupenda,
Kutufariji sisi wana wako,
Umeinua watumishi wako,
Kutufariji katika shida zetu,**

Tunakuomba Mungu Baba yetu,
Utupe neema sisi wana wako,
Kutufariji pia na kiroho,
Ili tuishi kwa imani yako,
**Na Mungu wetu anawatafuta,
Walio tayari kufanya kazi naye
Kututunza sisi wana wake,
Kwani yeye ni baba wa yatima x2**

Ooh! Sisi sio yatima tena (tunaye baba)

Sisi sio yatima tena (tunaye baba)

Ooh! Anatumunza baba, anatumunza baba

Anatulisha baba, anatupenda baba x2

Anatupenda baba, anatulinda baba

Anatutunza baba, anatupenda baba

WEWE NI BABA WA YATIMA

Wewe ndiwe baba wa yatima ooh! Tena Mume wa wajane x2

Tunakuabudu baba, tunakuheshimu baba, hakika wewe ni baba yetu. X2

Pokea shukrani zetu baba ooh! Tena uwe mlinzi wetu, x2

Umetupa akili, umetupa na nguvu, hakika wewe ni baba yetu x2

Macho yetu na masikio, ooh! Yakutazame tukusikie x2

Wewe u mwema baba, ni kimbilio, hatuna mwingine ila ni wewe x2

SIKIA

sikia mwenzangu nikunong'oneze

Habari za huyu mwenye nguvu zote, mamlaka yote, mwokozi wa watu wote, mfalme wa wafalme

Anakuita uondoke huko uliko ni dhambinix2

Nenda usichelewe nenda,

Ni Yesu mwokozi mwana wa Mungu, mfariji wetu mleta wokovu sote twaokolewa kwa jina la Yesu.

